



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA

Tovuti: [www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz)



## TANGAZO

**KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA MAOMBI YA USAJILI WA AWALI KWA  
WANAOTARAJIA KUANZA MAFUNZO YA UTARAJALI (INTERNISHIP) MWEZI  
APRILI 2023**

Baraza la Wataalam wa Maabara linachukua nafasi hii kuwajulisha Wataalam wote waliohitimu shahada ya Sayansi ya Maabara za Afya kuwa dirisha la maombi ya usajili wa awali limefunguliwa leo Tarehe 01.03.2023

Wahitimu wote wa Shahada ya Sayansi ya Maabara za Afya ya Binadamu (Medical/Health Laboratory Sciences) ambao bado hawajafanya mafunzo ya vitendo (utarajali) na wanaotarajia kuanza mafunzo haya mwezi Aprili 2023 wanatakiwa kufanya maombi ya usajili wa awali kwenye mfumo wa [hprs.moh.go.tz](http://hprs.moh.go.tz) ili kuwawezesha kufanya maombi ya utarajali pindi dirisha litakapofunguliwa.

Vile vile wataalam ambao walishafanya mitihani ya usajili lakini hawajafanya maombi ya **usajili wa kudumu** wanasisitizwa kufanya maombi ya usajili wa kudumu kabla dirisha halijafungwa ili kuepuka changamoto za kubadilika kwa mahitaji ya mfumo wa HPRS kama iliyoielezwa kwenye matangazo yaliyopita.

Wataalam wote ambao hawajafanya mitihani ya usajili au walifeli, ambao waliopata usajili wa awali nje ya mfumo wa HPRS wanasisitizwa kutuma taarifa zao ili kuingizwa kwenye [hprs.moh.go.tz](http://hprs.moh.go.tz) ili kuwawezesha kufanya maombi ya mitihani ya usajili pindi dirisha likifunguliwa.

Mwisho wa Maombi haya ni Tarehe 12.03.2023

**Baraza Halitahusika na usumbufu utakaojitokeza baada ya Dirisha kufungwa**

Upatapo tangazo hili mtaarifu na mwenzako.

Kwa Maelezo piga simu 0734005777

Imetolewa na

Ofisi ya Msajili

Baraza la Wataalam wa Maabara

